


# MAAZIMIO YA WANANCHI KWA VYAMA VYA SIASA KUHUSU UHIFADHI WA MISITU NA MAZINGIRA: UCHAGUZI WA 2015

Imetolewa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa kushirikiana na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kupitia mradi wa Haki Katika Misitu Tanzania kwa ufadhili wa Programu ya Uwajibikaji Tanzania.

**Juni 2015**

# Yaliyomo

**Muhtasari Mahususi** ... **iii**

**1.0 Utangulizi** ... **1**

1.1 Kuhusu Misitu nchini ... 1

1.2 Kuhusu MJUMITA ... 1

1.3 Malengo ya maazimio ya wananchi kuhusu Uhifadhi wa Misitu na Mazingira. ... 2

**2.0 Umuhimu wa misitu yetu** ... **2**

**3.0 Hali ya misitu kwa sasa** ... **3**

**4.0 Uchaguzi mkuu 2015 na mustakabali wa misitu yetu** ... **4**

4.1 Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa changamoto za misitu na mapendekezo ya kutatua changamoto hizo ... 4

4.2 Changamoto zilizoibuliwa na mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo. ... 6

4.2.1 Sera na Sheria ya misitu kutotekelezwa kwa vitendo ... 6

4.2.2 Serikali kutokutoa kipaumbele kwenye uwekezaji katika sekta ya misitu. ... 6

4.2.3 Siasa kuingilia shuguli za uhifadhi wa misitu ... 7

4.2.4 Migogoro ya ardhi ... 7

4.2.5 Uvunaji holela wa rasilimali za misitu ... 8

4.2.6 Elimu ndogo ya umuhimu wa misitu na mazingira kwa jamii na umma ... 8

4.2.7 Kilimo na Ufugaji kwa njia za mazoea ... 9

4.2.8 Uharibifu wa misitu kutokana na utafutaji wa nishati ya mkaa na Kuni ... 9

4.2.9 Utawala dhaifu katika sekta ya misitu kwenye baadhi ya maeneo ... 11

4.2.10 Utegemezi mkubwa wa jamii kwenye mazao ya misitu ... 11

**5.0 Hitimisho** ... **12**

# Muhtasari Mahususi

Misitu ni rasilimali muhimu sana ambayo nchi yetu imejaliwa. Inakadiriwa Tanzania ina misitu yenye ukubwa wa hekta milioni 48.1 ambayo ni sawa na asilimia 38 ya eneo lote la ardhi ya nchi yetu. Misitu hii hata hivyo inakabiliwa na upoteaji wa kiwango cha eneo la hekta 400,000 kwa mwaka, na hii inasababishwa na kilimo cha kuhama hama, mifugo, moto na uvunaji holela na usio endelevu wa mazao ya misitu na shughuli zingine za kibinadamu.

Kutokana na changamoto zinazoikabili misitu na jamii inayoishi pembezoni mwa misitu, jamii imeamua kuandaa majumuisho ya changamoto hizo na mapendekezo ya namna ya utatuzi wake. Lengo ni kutumia fursa ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 katika utatuzi wa changamoto za misitu na jamii ili misitu yetu iendelee kutoa huduma ya kiikolojia, kiuchumi na kijamii kwa muda mrefu.

MJUMITA kupitia mikutano yake ya mwaka ya mitandao ilikusanya maoni ya wanajamii kuona ni kwa namna gani itatumia fursa ya uchaguzi wa 2015 katika kutatua changamoto wanazokabiliana nazo katika kuhifadhi na kusimamia misitu. Maoni yamekusanywa katika mikutano 76 ya mitandao ambayo imehusisha vijiji 297 katika Wilaya 23 na Mikoa 13 Tanzania Bara. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

1. Sera na Sheria ya misitu kutotekelezwa kwa vitendo.
2. Serikali kutokutoa kipaumbele katika uwekezaji kwenye sekta ya misitu.
3. Siasa kuingilia shughuli za uhifadhi wa misitu.
4. Migogoro ya ardhi.
5. Uvunaji holela wa rasilimali za misitu.
6. Elimu ndogo ya umuhimu wa misitu na mazingira kwa jamii na umma.
7. Kilimo na ufugaji kwa njia za mazoea.
8. Uharibifu wa misitu kutokana na utafutaji wa nishati ya mkaa na kuni.
9. Utawala dhaifu katika sekta ya misitu.
10. Utegemezi mkubwa wa jamii kwenye mazao ya misitu.

Baadhi ya mapendekezo ya kutatua changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

- Kuhakikisha Sera na Sheria ya misitu inatekelezwa kwa vitendo.
- Kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji.
- Kusisitiza uboreshwaji wa utawala na uwajibikaji katika sekta ya misitu kwenye ngazi zote.

Mchakato huu umetekelezwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa kushirikiana na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG).

# 1.0 Utangulizi

## 1.1 Kuhusu Misitu nchini

Misitu ni rasilimali muhimu sana ambayo nchi yetu imejaaliwa. Inakadiriwa Tanzania ina misitu yenye ukubwa wa hekta milioni 48.1 ambayo ni sawa na asilimia 38 ya eneo lote la ardhi ya nchi yetu. Asilimia 31 ya misitu yote ipo chini ya uhifadhi, katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ngazi ya Serikali Kuu, Serikali za Wilaya na Serikali za Vijiji. Asilimia 69 ya misitu iliyobaki ipo katika ardhi za Vijiji na kwenye maeneo ya wazi (general land).

Kwa sasa kuna misitu takribani 600 inayosimamiwa na Serikali Kuu na misitu takribani 200 inayosimamiwa na Serikali za Wilaya, takribani misitu 71 ipo chini ya Serikali za Vijiji na misitu takribani 409 ipo katika hatua nzuri ya kutangazwa kuwa misitu chini ya usimamizi wa Serikali za Vijiji (Chanzo: Tovuti ya Serikali, June 2015.)

Misitu hii hata hivyo inakabiliwa na upoteaji wa kiwango cha eneo la hekta 400,000 (Chanzo: Ripoti ya NAFORMA, 2013) kwa mwaka, na hii inasababishwa na kilimo cha kuhama hama, malisho ya mifugo, moto na uvunaji holela na usio endelevu wa mazao ya misitu na shughuli zingine za kibinadamu.

## 1.2 Kuhusu MJUMITA

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) ni shirika lisilo la kiserikali lililoanzishwa mwaka 2000 na kusajiliwa mwaka 2007 kwa usajili nambari 00NGO/1119. MJUMITA ina jumla ya mitandao 116 katika ngazi ya kata ikiwa na jumla ya wanachama 10,343 katika kanda sita za kitaifa, kanda hizo ni kanda ya Kati, Mashariki, Magharibi, Kaskazini, Kusini na Nyanda za juu Kusini. Miradi yetu imekuwa ikilenga kuzisaidia jamii ziishizo kandokando mwa misitu kushiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa misitu, kuongeza kipato kupitia uanzishwaji wa VICOBA, Kuanzisha miradi mbadala kwa ajili ya jamii hasa ufugaji wa nyuki, ufugaji samaki, ufugaji vipepeo, kilimo cha uyoga na kuboresha njia za kilimo kwa ujumla ili jamii ziishizo pembezoni mwa misitu kuacha kilimo cha kuhamahama na uchomaji moto hovyo. Tunafanya kazi katika vijiji 452, Kata 143, Wilaya 30 na Mikoa 13 na tunawawezesha wananchi hao kusimamia misitu yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 1,800,000.

### 1.3 Malengo ya maazimio ya wananchi kuhusu Uhifadhi wa Misitu na Mazingira.

Malengo makuu ya maazimio haya ni pamoja na:

1. Kutoa msukumo zaidi kwa Serikali na viongozi wa kuchaguliwa katika kusimamia uhifadhi mzuri wa misitu ya asili.
2. Kusaidia viongozi wa kuchaguliwa kutambua kwa kina umuhimu na changamoto mbalimbali za uhifadhi wa misitu na jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu ili kuwashawishi kuchukua hatua madhubuti pindi watakapochaguliwa.

## 2.0 Umuhimu wa misitu yetu

Misitu yetu ina manufaa mengi Kitaifa na Kimataifa na inachangia kwa kiasi kikubwa kiuchumi, kiikolojia na kijamii: Mfano

1. Misitu ni vyanzo vya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika sekta mbalimbali, kwa mfano misitu ya Udzungwa Scarp ni chanzo kikubwa cha maji yanayotumika kwa shughuli za kilimo katika bonde la Kilombero. Misitu ya Malindi maji ni vyanzo vikubwa vya maji yanayotumika katika miji mbalimbali nchini. Aidha asilimia 40 ya umeme wetu unategemea vyanzo vya maji.
2. Misitu husaidia katika uhifadhi wa udongo na kuzuia maporomoko ya ardhi ambayo yanaweza kuleta athari kubwa kwa jamii ikiwa ni pamoja na uharibifu wa miundombinu.
3. Misitu husaidia katika unyonyaji wa hewa ukaa inayosababisha mabadiliko tabia nchi na hivyo kusaidia nchi na dunia kwa ujumla katika jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko tabia nchi.
4. Misitu ni makazi ya viumbe hai ambao ni muhimu katika mnyororo wa kiikolojia. Baadhi ya viumbe hao ni adimu sehemu nyingine duniani na hivyo kutupa fursa ya utalii.
5. Misitu ni vyanzo mbalimbali vya huduma muhimu za kijamii kama upatikanaji wa dawa za asili, vyakula vya asili, upatikanaji wa mbao na miti kwa ajili ya ujenzi na upatikanaji wa nishati kwa ajili ya shughuli mbali mbali hasa katika vijiji vyetu.

## 3.0 Hali ya misitu kwa sasa

Pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali na wadau wengine ikiwa ni pamoja na wanavijiji na mashirika yasiyo ya kiserikali, bado hali ya misitu yetu ni mbaya. Inakadiriwa Tanzania hupoteza wastani wa hekta 400,000 za misitu kila mwaka (Ripoti ya Naforma 2013). Upotevu huu husababishwa kwa kiasi kikubwa na mambo yafuatayo:

1. Kilimo cha kuhamahama kinachosababisha ufyekaji wa misitu, kinachosababishwa na wakulima kutafuta rutuba na unyevu wa udongo.
2. Uchomaji wa misitu hovyo. Changamoto hii huchangiwa na mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na (1).Uandaaji wa mashamba kwa kutumia mioto, (2). Imani potofu zinazohusisha uchomaji wa eneo kubwa na umri wa kuishi wa mchomaji na (3). Shughuli za uvunaji asali na uwindaji usiofuata njia bora.
3. Umiliki wa mifugo unaozidi uwezo wa maeneo maalumu ya malisho. Kwa miaka ya karibuni ufugaji holela wa mifugo umekuwa tishio kubwa kwa misitu na kilimo, na maeneo mengi ya misitu ambayo yamekosa usimamizi mzuri yako mbioni kuwa jangwa. Mfano msitu wa Masito mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Uvinza

Changamoto nyingine za misitu ni pamoja na:

1. Uvamizi wa misitu kwa ajili ya makazi, mfano mzuri ni uvamizi katika misitu ya asili ya Pugu na Kazimzumbwi mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.
2. Uvunaji haramu wa miti kwa ajili ya magogo, mbao, kuni na uchomaji holela wa mikaa.
3. Uchimbaji haramu wa madini ndani ya misitu ya hifadhi umekuwa ukichangia uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji.

# 4.0 Uchaguzi mkuu 2015 na mustakabali wa misitu yetu

## 4.1 Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa changamoto za misitu na mapendekezo ya kutatua changamoto hizo

Kwa sababu changamoto nyingi za misitu yetu zinatokana na kukosekana kwa uwajibikaji, usimamizi dhaifu wa sera na sheria, rushwa na ufinyu wa bajeti, MJUMITA kupitia mikutano yake Mikuu ya kila mwaka (kuanzia mwaka 2000 mpaka 2014) imekuwa ikitoa mapendekezo kwa watunga sera na wafanya maamuzi ya jinsi ya kuboresha hali ya misitu nchini. Vile vile WanaMJUMITA kutoka mitandao 74 walipata fursa ya kukutana kipindi cha kati ya mwezi Mei na Juni mwaka 2015 kutafakari ni kwa namna gani changamoto hizi za misitu zinaweza kupewa kipaumbele kupitia fursa ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Mitandao ya MJUMITA ilikutana katika mikutano yao mikuu ya kila mwaka (idadi ya mitandao iliyokutana kwa kila kanda imeainishwa katika jedwali nambari 1 hapo chini) na kutafakari changamoto mbali mbali za misitu wanazokabiliana nazo kila siku katika shughuli zao za uhifadhi wa misitu.

### *Jedwali 1 likionesha jumla ya mitandao kwa kanda na changamoto zilizoibuliwa kwa kila kanda*

| Kanda | Jumla ya Mitandao | Changamoto |
|---|---|---|
| Kati | 15 (vijiji 50) | Usimamizi shirikishi wa misitu: Kukosekana kwa motisha kwa wananchi wanaoshiriki katika uhifadhi wa misitu, kutosainiwa kwa mikataba ya usimamizi wa pamoja wa misitu<br>Kilimo na ufugaji wa mazoea<br>Umasikini wa jamii jirani na misitu<br>Uwekezaji mdogo wa Serikali katika sekta ya misitu |

| | | |
|---|---|---|
| Mashariki | 10 (vijiji 31) | Usimamizi shirikishi wa misitu: Kukosekana kwa motisha kwa wananchi wanaoshiriki katika uhifadhi wa misitu, kutosainiwa kwa mikataba ya usimamizi wa pamoja wa misitu<br>Migogoro ya ardhi<br>Uvunaji holela wa mazao ya msitu<br>Utawala dhaifu katika sekta ya misitu<br>Kilimo na ufugaji wa mazoea |
| Magharibi | 7 (vijiji 21) | Umasikini wa jamii jirani na misitu<br>Kilimo na ufugaji wa mazoea<br>Uwekezaji mdogo wa Serikali katika sekta ya misitu<br>Migogoro ya ardhi<br>Kilimo na ufugaji wa mazoea |
| Kaskazini | 16 (vijiji 72) | Usimamizi shirikishi wa misitu: Kukosekana kwa motisha kwa wananchi wanaoshiriki katika uhifadhi wa misitu, kutosainiwa kwa mikataba ya usimamizi wa pamoja wa misitu<br>Utawala dhaifu katika sekta ya misitu<br>Uvunaji holela wa mazao ya misitu |
| Kusini | 12 (vijiji 60) | Utawala dhaifu katika sekta ya misitu<br>Usimamizi shirikishi wa misitu: Kukosekana kwa motisha kwa wananchi wanaoshiriki katika uhifadhi wa misitu, kutosainiwa kwa mikataba ya usimamizi wa pamoja wa misitu<br>Uwekezaji mdogo wa Serikali katika sekta ya misitu |
| Nyanda za Juu Kusini | 14 (vijiji 62) | Migogoro kati ya wananchi na wanyamapori<br>Uwekezaji mdogo wa Serikali katika sekta ya misitu<br>Umasikini wa jamii jirani na misitu<br>Utawala dhaifu katika sekta ya misitu |

Jumla ya mitandao 74 kutoka vijiji 297 katika Wilaya 23 ilikutana na kujadili changamoto mbalimbali za misitu katika maeneo yao na mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Wajumbe walioshiriki ni pamoja na wenyeviti wa vijiji, watendaji wa vijiji na kata, waheshimiwa madiwani, viongozi wa kamati za maliasili za vijiji, wanachama wa MJUMITA kutoka vikundi mbali mbali katika ngazi za vijiji ikiwa ni pamoja na vikundi vya wafugaji, vikundi vya hisa, vikundi vya mazingira na Maafisa Misitu wa Wilaya. Jumla ya changamoto 10 kubwa ziliibuliwa na wanamitandao. Wanamitandao pia walitoa mapendekezo kadhaa ya namna nzuri Serikali na viongozi watakaochaguliwa kwenye uchaguzi mkuu 2015 watakavyozishughulikia changamoto hizo za misitu nchini.

## 4.2 Changamoto zilizoibuliwa na mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

### 4.2.1 Sera na Sheria ya misitu kutotekelezwa kwa vitendo

Sera na Sheria za misitu nchini zinatambua na kusisitiza Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Hata hivyo kumekuwa na changamoto kubwa kwenye utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Kwa mfano, ukosefu wa mikataba kati ya Vijiji na Serikali katika usimamizi wa misitu, kutokuwepo kwa uwazi kwenye ugawanaji wa majukumu na faida kati ya Vijiji na Serikali zimekuwa zikitajwa kama vikwazo vikubwa kwenye utekelezaji wa usimamizi wa pamoja wa misitu. Hivyo tunapendekeza Serikali na viongozi watakaochaguliwa kuchukua hatua zifuatazo:

1. Kuhakikisha Sera na Sheria ya misitu inatekelezwa kwa vitendo hasa usimamizi shirikishi wa misitu.
2. Kuwajengea uwezo wanavijiji kusimamia misitu ya Serikali kuu ambayo inaendelea kuharibika katika maeneo mengi nchini.
3. Kutoa motisha kwa jamii zinazoshiriki kusimamia misitu ya jamii kwa kubakisha mapato yanayotokana na mazao ya misitu kwa asilimia mia (100%).

### 4.2.2 Serikali kutokutoa kipaumbele kwenye uwekezaji katika sekta ya misitu.

Kutokana na umuhimu wake kwenye sekta nyingine, tunapendekeza sekta ya misitu ipewe kipaumbele katika bajeti kama sekta za afya, elimu na kilimo. Hii itasaidia:

1. Sekta ya misitu Tanzania kuendelea kuchangia uchumi wa nchi kwa muda mrefu zaidi. Tukumbuke kuwa sekta nyingi nchini

zinategemea sekta ya misitu kujiendesha. Mfano kilimo cha umwagiliaji, sekta ya maji, sekta ya nishati ya umeme, viwanda, utalii na sekta nyingine nyingi zinategemea maji ambayo vyanzo vyake ni katika misitu.

2. Jamii zinazozunguka misitu kupata elimu za mara kwa mara juu ya umuhimu wa misitu na hivyo kushiriki katika kuilinda misitu yetu vizuri zaidi.
3. Kuwezesha wananchi kuanzisha vitalu vya miti na upandaji wa miti katika maeneo yao ili wasiwe wategemezi katika misitu ya asili.

### 4.2.3 Siasa kuingilia shuguli za uhifadhi wa misitu

Kumekuwa na desturi ya baadhi ya wanasiasa kutoa kauli zinazokinzana na sheria na sera za misitu. Baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitoa matamko na ahadi (hasa wakati wa uchaguzi) kwamba kwa nafasi zao watashawishi shughuli za kibinadamu kuruhusiwa katika maeneo ya hifadhi za misitu. Kauli za namna hiyo zimekuwa na athari kubwa kwenye juhudi za uhifadhi wa misitu nchini ikiwa ni pamoja na baadhi ya misitu kuvamiwa na wananchi. Wanamtandao tunataka Serikali na viongozi watakaochaguliwa:

1. Kukemea wanasiasa na viongozi wengine watakaotoa kauli zitakazokinzana na sera na sheria za misitu.
2. Kuwachukulia hatua viongozi ambao kwa kauli na matendo yao wamesababisha/wanasababisha kuvamiwa na kuharibiwa kwa misitu ya asili.

### 4.2.4 Migogoro ya ardhi

Migogoro ya ardhi kati ya vijiji na vijiji, vijiji na hifadhi za misitu na wanyama pori imekuwa ikiongezeka nchini siku hadi siku. Migogoro hii imekuwa na athari mbali mbali katika juhudi za uhifadhi ikiwa ni pamoja na kujenga chuki kwa wananchi juu ya masuala ya uhifadhi na hivyo kuzorotesha juhudi za Serikali katika uhifadhi hasa kupambana na ujangili. Hivyo tunaitaka Serikali na viongozi watakaochaguliwa:

1. Kuhakikisha kunakuwepo na mipango na mikakati madhubuti itakayozuia kutokea kwa migogoro ya ardhi ya mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya vijiji kufanyiwa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi.

2. Kuhakikisha kuwa Serikali na viongozi wanatoa kipaumbele katika kushughulikia migogoro kwa wakati ili kuepusha athari za migogoro ya ardhi katika mazingira na kwa binadamu hasa vifo.

3. Kuhakikisha kuwa Serikali inakabiliana na wanyama waharibifu kwa wakati ili kuzuia athari kubwa kwenye mazao na mali za wananchi. Aidha, ili wananchi waendelee kupenda shughuli za uhifadhi, Serikali ihakikishe kuwa inatoa fidia inayozingatia hasara halisi ya uharibifu kwa watu walioathirika.

### 4.2.5 Uvunaji holela wa rasilimali za misitu

Kumekuwa na uvunaji haramu wa mazao ya misitu hasa mbao, kuni na mkaa katika misitu ya vijiji, maeneo ya wazi na misitu ya Serikali Kuu. Uvunaji haramu unatishia kutoweka kwa baadhi ya misitu muhimu nchini kama misitu ya Kazimzumbwi na Pugu. Uharibifu wa misitu umekuwa pia ukichangia uzalishaji wa gesi ukaa inayosababisha mabadiliko tabianchi, na kuleta athari kama vile ukame, mafuriko na ongezeko la joto. Hivyo, tunaitaka Serikali na viongozi watakaochaguliwa kuchukua hatua zifuatazo:

1. Kutekeleza Sera na Sheria na kuandaa mipango ya Wilaya ya uvunaji wa mazao ya misitu ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uvunaji endelevu wa mazao ya misitu kwenye misitu ambayo shughuli za uvunaji zinakubalika kisheria.

2. Kutoa elimu kwa wananchi juu ya mipango na utaratibu wa uvunaji wa mazao ya misitu.

3. Kuhakikisha Sera na Sheria za uvunaji endelevu wa misitu zinatambua umuhimu wa wananchi katika shughuli za uhifadhi. Hivyo jamii zinazoshiriki katika shughuli za uhifadhi zinapata mgao wa moja kwa moja wa manufaa yanayotokana na mauzo ya mazao ya misitu yaliyovunwa katika maeneo yao.

### 4.2.6 Elimu ndogo ya umuhimu wa misitu na mazingira kwa jamii na umma

Bado kuna umuhimu wa jamii na umma kwa ujumla kupata elimu za mara kwa mara kuhusu uhifadhi wa misitu na mazingira. Hii inatokana na ukweli kwamba mbinu za uhifadhi wa misitu na mazingira zinabadilika mara kwa mara. Hivyo tunataka viongozi na Serikali itakayochaguliwa kuchukua hatua zifuatazo:

1. Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu za uhifadhi wa misitu na mazingira kwa jamii, hasa kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi, matumizi bora ya ardhi, matumizi endelevu ya misitu na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

2. Kuingiza somo la mazingira kwenye mtaala wa shule za msingi na sekondari. Hii itasaidia kuwa na jamii yenye uelewa mpana kuhusu masuala ya mazingira na hivyo kushiriki katika kulinda na kuyatetea mazingira yasiharibiwe.

### 4.2.7 Kilimo na Ufugaji kwa njia za mazoea

Kilimo na ufugaji kwa njia za mazoea kimekuwa na athari kubwa katika uhifadhi nchini. Kilimo cha kuhamahama kinachangia kwa zaidi ya asilimia 50 ya uharibifu wa misitu (Luoga, 2000).

Ufugaji wa kuhamahama nao umekuwa na athari kubwa kwenye uhifadhi wa misitu na bionuai za misitu. Kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi iliyosababisha maeneo mengi ya wafugaji kuwa makame, wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo ndani ya hifadhi za misitu kwa ajili ya malisho na maji. Tunaitaka Serikali na viongozi watakaochaguliwa kutekeleza yafuatayo:

1. Kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji.

2. Kuboresha Sera na Sheria za kilimo na mifugo ili kusisitiza njia bora zaidi za kilimo na ufugaji kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo.

3. Kuwekeza (Hasa kutenga bajeti) zaidi katika njia bora za kilimo na ufugaji kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo.

4. Kuratibu masuala mtambuka yanayoathiri sekta ya misitu mfano kilimo na mifugo.

5. Masuala ya kilimo na ufugaji bora yawe ni agenda ya kudumu kwenye mikutano ya wananchi.

### 4.2.8 Uharibifu wa misitu kutokana na utafutaji wa nishati ya mkaa na Kuni

Asilimia 96 ya kaya nchini hutumia kuni au mkaa. Asilimia 91 ya kaya jijini Dar es Salaam hutumia mkaa kama nishati ya kupikia. Inakadiriwa kuwa biashara ya mkaa na kuni iliingiza takribani shilling trillion 1.6 ya mapato toka kwa zaidi ya watu 300,000 ambao ni wachomaji wa mkaa, wasafirishaji na wafanya biashara wa mkaa kwa mwaka 2012.

Hivyo kuna umuhimu wa kutafuta njia ambayo itahakikisha wananchi wanapata nishati ya mkaa na kuni kwa namna ambayo haitakuwa na athari katika misitu na mazingira. Miradi ya mkaa endelevu nchini imeonesha kuwa mkaa unaweza kuzalishwa kwa njia endelevu ukawa na faida kwa wananchi kwa kupata nishati, kupata kipato, kupata ajira, Serikali kupata kodi na wakati huo huo kuhakikisha uhifadhi mzuri wa misitu na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Hivyo tunaitaka Serikali na viongozi watakaochaguliwa kuchukua hatua zifuatazo;

1. Kubadilisha mtazamo kuwa nishati ya kuni na mkaa ni nishati duni na ya asili hivyo kutoona fursa zilizopo kuiendeleza kwa teknologia za kisasa.
2. Kutetea kuanzishwa na kutekelezwa kwa Sera na Sheria zitakazo elekeza namna ya uzalishaji wa mkaa na kuni kwa njia endelevu.
3. Kuwa na mikakati madhubuti ya kutenga maeneo maalum ya kupanda miti na misitu kwa ajili ya kuzalisha kuni na mkaa kwa njia endelevu.
4. Kuendeleza na kuboresha teknolojia sahihi na za gharama nafuu za upatikaji na utumiaji wa nishati mfano majiko sanifu, matanuri yaliyoboreshwa na biogesi.

### 4.2.9 Utawala dhaifu katika sekta ya misitu kwenye baadhi ya maeneo

Kumekuwa na viongozi na watumishi wa Serikali wasiokuwa waaminifu na hivyo kushiriki katika vitendo vya kuhujumu misitu hasa katika ngazi za vijiji na Wilaya. Baadhi ya viongozi na watumishi wa Serikali wamekuwa wakishirikiana na wavunaji haramu kuvuna mazao ya misitu isivyo halali. Baadhi ya viongozi wamekuwa wakitoa vibali visivyo halali (feki) kwa ajili ya uvunaji, wamekuwa wakipokea rushwa na kuruhusu uvunaji zaidi ya idadi ya uvunaji ulioandikwa kwenye vibali halali, wamekuwa wakikamata wahalifu na kuwaachia baada ya kupokea rushwa kutoka kwa watuhumiwa. Hivyo tunataka Serikali na viongozi watakao chaguliwa kuchukua hatua zifuatazo:

1. Kusisitiza kuboreshwa kwa hali ya utawala na uwajibikaji katika sekta ya misitu kwa ngazi zote kutoka ngazi za vijiji mpaka Serikali kuu.
2. Kusimamia sheria, sera, kanuni na taratibu za uhifadhi wa misitu kwa vitendo kwa kuhakikisha wahalifu wa misitu wanafikishwa katika vyombo vya sheria.

3. Kuhakikisha viongozi na watumishi wanaoshiriki kuhujumu misitu wanachukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani badala ya kuhamishwa vituo vyao vya kazi kama inavyofanyika sasa.

### 4.2.10 Utegemezi mkubwa wa jamii kwenye mazao ya misitu.

Pamoja na sababu nyingine, umasikini wa jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa misitu nchini. Jamii hizi zikisaidiwa kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi itasaidia kuondoa utegemezi katika mazao ya misitu na hivyo kuchangia katika uhifadhi mzuri wa misitu yetu. Kwa mfano, Tanzania ina fursa kubwa ya uzalishaji wa asali na nta, inakadiriwa uwezo wa Tanzania katika uzalishaji wa asali ni tani 138,000 na nta ni tani 9,200, lakini asali inayozalishwa kwa sasa ni wastani wa tani 4,860 na nta tani 340 tu.. Hii ni sawa na asilimia 3.5 tu ya uwezo wa nchi katika uzalishaji wa asali. Tunataka Serikali na viongozi watakaochagulia kusisitiza yafuatayo.

1. Kuzisimamia kikamilifu idara na mamlaka zinazohusika kuhakikisha kwamba jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu zinajengewa uwezo na kusaidiwa kuanzisha miradi midogo midogo ya maendeleo ili kupunguza utegemezi wa jamii hizo katika misitu.

2. Kuzisimamia idara na mamlaka husika kushirikiana na jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu kutumia fursa ya asali na nta kuzalisha kwa wingi, kuongeza thamani ya asali na nta na kutafuta masoko ya uhakika ili jamii na Serikali kunufaika zaidi na shughuli za uhifadhi wa misitu nchini.

## 5.0 Hitimisho

Changamoto zote za misitu zinaweza kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu na viongozi wenye dhamira ya kweli ya kufanya hivyo. Tunawaomba viongozi watakaochaguliwa kuwa na dhamira ya kweli ya kutatua changamoto za misitu ili kuweza kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi na misitu yetu iendelee kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa muda mrefu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadae.

## DIRA YA MJUMITA

MJUMITA inataka kuona jamii inayojali, inayosimamia, inayotumia misitu na mazao ya misitu kwa uendelevu

## MWELEKEO WA MJUMITA

MJUMITA itajitahidi kufikia dira yake kwa kuhamasisha, kuwajengea uwezo na kuunganisha jamii na mitandao ya jamii kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa wadau katika ushawishi na ufanyaji wa maamuzi juu ya umiliki, usimamizi na utunzaji wa misitu.

**Kwa mawasiliano**

**MJUMITA**

S.L.P 21522, Dar-es-salaam-Tanzania,
Simu: 255222669007,
Barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org